

KUMB: PPR/17 - 11/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 1 NOVEMBA 2017**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Novemba 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Oktoba 2017. Kwa mwezi Novemba 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 55/lita (sawa na asilimia 2.69), Shilingi 46/lita (sawa na asilimia 2.43) na Shilingi 81/lita (sawa na asilimia 4.35) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 55.49/lita (sawa na asilimia 2.84), Shilingi 46.36/lita (sawa na asilimia 2.58) na Shilingi 80.87/lita (sawa na asilimia 4.63) sawia. Ongezeko la bei za mafuta kwenye soko la ndani, limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia, na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununulia mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote katika mkoa wa Tanga nazo zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Oktoba 2017. Ikumbukwe kwamba, katika mkoa wa Tanga, mzungu mpya wa mafuta kupokelewa kabla ya Oktoba 2017 ulipokelewa mwezi Agosti 2017 na hivyo, bei za mafuta zilizokuwa zinatumiwa mwezi Oktoba 2017 zilianza kutumika tangu mwezi Septemba 2017. Kwa mwezi Novemba 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 112/lita (sawa na asilimia 5.60), Shilingi 122/lita (sawa na asilimia 6.52) na Shilingi 128/lita (sawa na asilimia 7.10) sawia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 111.57/lita (sawa na asilimia 5.93), Shilingi 122.44/lita (sawa na asilimia 6.93) na Shilingi 128.49/lita (sawa na asilimia 7.56) sawia. Ongezeko la bei za mafuta mkoani Tanga limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia, na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununulia mafuta.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.****
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti cha wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,118	1,954	1,939
Arusha	2,161	2,056	1,995
Arumeru (Usa West)	2,161	2,056	1,995
Karatu	2,179	2,074	2,013
Monduli	2,166	2,061	2,000
Monduli-Makuyuni	2,171	2,066	2,005
Ngorongoro (Loliondo)	2,245	2,140	2,079
Kibaha	2,123	1,959	1,944
Bagamoyo	2,129	1,965	1,950
Kisarawe	2,126	1,961	1,946
Mkuranga	2,128	1,964	1,949
Rufiji	2,146	1,982	1,967
Dodoma	2,177	2,013	1,998
Bahi	2,184	2,020	2,005
Chemba	2,203	2,039	2,024
Kondoa	2,210	2,045	2,030
Kongwa	2,174	2,010	1,995
Mpwapwa	2,178	2,014	1,999

Iringa	2,182	2,018	2,003
Kilolo	2,187	2,023	2,007
Mufindi (Mafinga)	2,192	2,028	2,013
Njombe	2,210	2,046	2,031
Ludewa	2,248	2,084	2,069
Makete	2,241	2,077	2,062
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,208	2,044	2,029
Bukoba	2,333	2,169	2,154
Biharamulo	2,308	2,143	2,128
Karagwe (Kayanga)	2,350	2,185	2,170
Kyerwa (Ruberwa)	2,355	2,191	2,176
Muleba	2,333	2,169	2,154
Ngara	2,299	2,135	2,119
Misenyi	2,342	2,177	2,162
Geita	2,283	2,119	2,104
Bukombe	2,272	2,108	2,093
Chato	2,304	2,140	2,125
Mbogwe	2,321	2,157	2,142
Nyang'hwale	2,298	2,134	2,119
Kigoma	2,349	2,185	2,170
Uvinza (Lugufu)	2,361	2,197	2,182
Buhigwe	2,338	2,174	2,159
Kakonko	2,306	2,142	2,127
Kasulu	2,335	2,171	2,156
Kibondo	2,314	2,149	2,134
Moshi	2,150	2,045	1,984
Hai (Bomang'ombe)	2,154	2,048	1,988
Mwanga	2,144	2,038	1,977
Rombo (Mkuu)	2,167	2,062	2,001
Same	2,137	2,031	1,971
Siha (Sanya Juu)	2,157	2,052	1,991
Lindi	2,177	2,013	1,998
Lindi-Mtama	2,195	2,031	2,016
Kilwa Masoko	2,152	1,988	1,973
Liwale	2,198	2,034	2,019
Nachingwea	2,206	2,042	2,027
Ruangwa	2,208	2,044	2,029
Babati	2,195	2,089	2,029
Hanang (Katesh)	2,205	2,100	2,039
Kiteto (Kibaya)	2,210	2,105	2,044
Mbulu	2,207	2,102	2,041
Simanjiro (Orkasumet)	2,227	2,121	2,061
Musoma	2,297	2,132	2,117
Musoma Vijijini (Busekela)	2,337	2,173	2,158
Rorya (Ingirijuu)	2,305	2,141	2,126

Rorya (Shirati)	2,340	2,176	2,161
Bunda	2,288	2,123	2,108
Butiama	2,293	2,129	2,114
Serengeti (Mugumu)	2,342	2,178	2,163
Tarime	2,308	2,143	2,128
Mbeya	2,225	2,061	2,046
Chunya	2,235	2,070	2,055
Chunya (Makongolosi)	2,249	2,085	2,070
Ileje	2,238	2,074	2,059
Kyela	2,241	2,077	2,062
Mbarali (Rujewa)	2,209	2,045	2,030
Mbozi (Vwawa)	2,235	2,070	2,055
Momba (Chitete)	2,243	2,079	2,064
Rungwe (Tukuyu)	2,234	2,070	2,055
Morogoro	2,143	1,979	1,964
Mikumi	2,159	1,995	1,980
Kilombero (Ifakara)	2,181	2,017	2,002
Kilombero (Mlimba)	2,203	2,039	2,024
Kilombero (Mngeta)	2,193	2,028	2,013
Ulanga (Mahenge)	2,192	2,027	2,012
Malinyi	2,202	2,038	2,023
Kilosa	2,162	1,997	1,982
Gairo	2,162	1,997	1,982
Mvomero (Wami Sokoine)	2,154	1,990	1,974
Turiani	2,168	2,004	1,989
Mtwara	2,191	2,026	2,011
Nanyumbu (Mangaka)	2,239	2,075	2,060
Masasi	2,216	2,052	2,037
Newala	2,223	2,058	2,043
Tandahimba	2,216	2,051	2,036
Mwanza	2,268	2,104	2,089
Kwimba	2,304	2,140	2,125
Magu	2,276	2,112	2,097
Misungwi	2,274	2,109	2,094
Sengerema	2,301	2,136	2,121
Ukerewe	2,328	2,163	2,148
Sumbawanga	2,291	2,127	2,112
Kalambo (Matai)	2,283	2,119	2,104
Nkasi (Namanyeke)	2,304	2,140	2,125
Katavi (Mpanda)	2,326	2,162	2,146
Mlele (Inyonga)	2,304	2,140	2,125
Songea	2,242	2,077	2,062
Mbinga	2,275	2,111	2,096
Namtumbo	2,271	2,107	2,091
Nyasa (Mbamba Bay)	2,277	2,113	2,098

Tunduru	2,300	2,136	2,121
Shinyanga	2,247	2,083	2,068
Kahama	2,261	2,096	2,081
Kishapu	2,275	2,111	2,096
Simiyu (Bariadi)	2,288	2,124	2,109
Busega (Nyashimo)	2,281	2,117	2,102
Itilima (Lagangabilili)	2,291	2,127	2,112
Maswa	2,280	2,116	2,100
Meatu (Mwanhuzi)	2,287	2,123	2,107
Singida	2,209	2,045	2,029
Iramba	2,221	2,057	2,042
Manyoni	2,193	2,029	2,014
Ikungi	2,204	2,040	2,025
Mkalama (Nduguti)	2,233	2,069	2,054
Tabora	2,272	2,108	2,093
Igunga	2,226	2,062	2,047
Kaliua	2,290	2,126	2,111
Ulyankulu	2,284	2,120	2,105
Nzega	2,237	2,073	2,057
Sikonge	2,284	2,120	2,105
Urambo	2,285	2,121	2,106
Tanga	2,104	1,999	1,938
Handeni	2,125	2,020	1,959
Kilindi	2,140	2,034	1,974
Korogwe	2,116	2,011	1,950
Lushoto	2,126	2,020	1,960
Mkinga (Maramba)	2,111	2,006	1,945
Muheza	2,109	2,004	1,943
Pangani	2,111	2,006	1,945

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,007.43	1,843.15	1,828.00

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	1,993.27	1,888.00	1,827.17

Mhandisi Godwin Samwel
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA